# Uhusika wa Kitoto katika Vibonzo Jongevu: Mbinu ya Kisanaa ya Kuivuta Hadhira ya Watoto

*Shadidu Abdallah*
*Chuo Kikuu cha St. John's cha Tanzania*

**Ikisiri**

**Makala haya yanajadili matumizi ya uhusika wa kitoto katika kazi za Vibonzo Jongevu na uumuhimu wake katika kuivuta hadhira ya watoto. Uchunguzi uliozaa makala haya uliongozwa na malengo makuu matatu. Mosi, kuchunguza mbinu za kitoto zinazotumika katika kazi za Vibonzo Jongevu. Pili, sababu za kutumika kwa mbinu hizo. Na tatu umuhimu wa mbinu hizo kwa hadhira ya watoto. Kazi teule zilizotumika ni za *Ubongo Kids, The Adventures of Abney and Teal* na *Dora the Explorer*. Uteuzi wa kazi hizi ulisukumwa na ukweli kuwa watunzi wake hutumia mbinu nyingi zenye mwegamo wa kitoto na hivyo kuivuta sana hadhira ya watoto. Utafiti uliongozwa na nadharia ya Mwitikio wa Msikilizaji ambapo mtafiti alitumia baadhi ya misingi ya nadharia katika kuchambua na kujadili data zake. Kwa jumla, imebainika kuwa watunzi wa Vibonzo Jongevu hutumia mbinu mbalimbali za kitoto katika utengenezaji wa kazi zao. Mbinu hizi ni pamoja na matumizi ya wahusika watoto, rangi za kuvutia, matendo ya kitoto, motifu za kitoto na uchanganyaji wa wahusika. Ni wazi kuwa, matumizi ya mbinu hizi yamelenga kuongeza idadi ya hadhira na mvuto wa sanaa kwa hadhira ya watoto.**

**Maneno Muhimu:** Uhusika, Uhusika wa Kitoto, Vibonzo Jongevu.

## Utangulizi

Watoto ni sehemu muhimu ya wanajamii yoyote ile duniani. Takwimu za kidunia kufikia mwaka 2018 zinaonesha kuwa watoto ni asilimia 27 ya watu wote duniani (UNICEF, 2018). Pamoja na mambo mengine, kundi hili lina fasihi yake maalum inayotofautiana na kundi la watu wazima n na watu wengine wote (Lyimo, 2014). Kwa msingi huo, toka hapo kale watunzi (wa kazi za uneni/simulizi na maandishi) wa kazi za watoto wamekuwa wakitumia vionjo maalum katika kazi za watoto ili kuifikia hadhira ya watoto. Katika namna zote mbili (masimulizi na maandishi) watunzi wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali kwa lengo la kuivuta hadhira na kuleta hali ya utoto katika kazi hizo.

Katika zama hizi za sayansi na teknolojia kumekuwa na ongezeko kubwa la kazi za watoto. Mbali ya Fasihi Simulizi na Andishi, hivi sasa ipo Fasihi ya Kidijiti/Kielektroniki (Abdallah, 2018., Mlaga, 2017., Mahenge, 2017). Kwa

namna ya kipekee kabisa fasihi hii inatengenezwa, inasambazwa, inauzwa, inahifadhiwa na kuwasilishwa kupitia vifaa vya kidijiti kama vile simu za mkononi, televisheni na ngamizi. Watoto ni wateja wakubwa wa kazi za kidijiti hasa *Vibonzo Jongevu v*ya kitoto. Moja ya sababu kubwa inayowavuta watoto kupenda kutazama kazi hizi ni namna watunzi wake walivyoweza kutumia mbinu maalum za kitoto kuivuta hadhira. Makala haya yanalenga kujadili kwa utondoti mbinu hizo na umuhimu wake katika ujenzi wa maudhui ya kazi husika.

## Wahusika

Ni viumbe au vitu anavyotumia msanii kuubeba ujumbe wake kwa lengo la kuuwasilisha kwa hadhira (Semzaba 2006, Madumulla, 2009). Wahusika wanaweza kuwa watu, wanyama, ndege, majini, mawe na miti. Mara nyingi wahusika huchorwa katika namna ya kujazilizana/kukamilishana (hasa kwa wahusika foili kwa mhusika mkuu) au katika namna ya kusuguana. Misuguano au maelewano ya wahusika ndiyo ambayo huisogeza mbele kazi ya msanii na kuibua maudhui. Mulokozi (2017) anaona kuwa misuguno ya wahusika hudhihirisha hisia, mawazo na misimamo ya wahusika. Hivyo, ili kazi ya msanii iwe nzuri na iweze kufikisha ujumbe kwa jamii ni muhimu wahusika wake wakachorwa vyema.

## Uhusika wa Kitoto

Katika makala haya dhana hii imechukuliwa kuwa ni ile hali ya kuwaumba wahusika katika namna ambayo wanafanana au kukaribiana kabisa na watoto. Uhusika wa kitoto unaweza kudhihirika katika namna mbalimbali; mfano, kupitia matendo, fikra, mazungumzo, mavazi, mawazo n.k. matumizi ya dhana *uhusika wa kitoto* haimaanisha kudogosha au kudharau uhusika wa watoto; bali inaelezea mbinu halisi za kisanaa zinazotumika kuwakilisha fikra, imani na matendo ya watoto kupitia kazi ya Fasihi.

## Vibonzo Jongevu

Fischer (1996) anadai kuwa, Vibonzo Jongevu ni filamu fupi (mara nyingi haizidi dakika sita) ya kidijiti ambayo mara nyingi huwalenga watoto na inayoonesha mfululizo wa matukio kwa kutumia wahusika wa kubuni. Vibonzo Jongevu ni sanaa mpya ambayo vimeibuka kutoka katika Vibonzo Tuli[1]. Kabla ya ujio wa Vibonzo Jongevu, jamii ilizoea matumizi ya Vibonzo Tuli kama sanaa iliyolenga

[1] Kwa mujibu wa Abdallah (2018), Vibonzo Tuli ni vibonzo vya kawaida ambavyo huchorwa katika vitabu, magazeti au katika kuta vikisawiri mambo mbalimbali katika jamii hasa jamii na siasa.

kuburudisha na kuelimisha (Mwashota na Chaula, 2016). Ujio wa Vibonzo Jongevu umeambatana na mabadiliko kadhaa ya kifani na kimaudhui. Kwa jumla, katika makala haya Vibonzo Jongevu vimejadiliwa kama kazi za watoto za kidijiti ambazo hutayarishwa, kuhifadhiwa na kuwasilishwa kwa kutumia vifaa vya kielektroniki kama vile televisheni, ngamizi na simu.

Kwa sehemu kubwa kazi za Vibonzo Jongevu huwalenga watoto. Malengo ya kazi hizi kama zilivyo kazi zingine za kisanaa ni kuiburudisha na kuielimisha jamii. Madumulla, (2001), Bakize (2014) na Chikaka (2017) wanaona kuwa, kisanaa, watoto ni hadhira yenye vionjo na mahitaji maalum ambayo hutofautiana sana na hadhira ya watu wazima. Pia, uundaji wa wahusika wake hutofautiana kwa kiwango fulani na wahusika wa kazi za watu wazima. Miongoni mwa mbinu inayotumika sana katika kuivuta hadhira ni uhusika wa kitoto ambapo wahusika huumbwa kwa namna ya kitoto ili kuivuta na kuifikia hadhira kwa urahisi.

## Ujitokezaji wa Uhusika wa Kitoto

Kama ilivyolezwa hapo awali, zipo mbinu maalum za kisanaa ambazo watunzi wa Vibonzo Jongevu huzitumia ili kuakisi dhana ya uhusika wa kitoto. Mbinu hizo hulenga kuivuta hadhira ya watoto ili iburudike na kuelimika**.** Hivyo basi, uhusika wa kitoto hujidhihirisha kwa kupitia mbinu zifuatazo:

## Matumizi Makubwa ya Rangi za Kuvutia

Inafahamika wazi kuwa watoto hupenda sana rangi hasa zile zenye kung'aa na kuvutia. Wataalamu wa masuala ya elimu na ujifunzaji wanasisitiza kuwa rangi husaidia sana watoto kujifunza mambo mbalimbali hasa katika hatua za awali za ujifunzaji. Vilevile, kwa upande wa fasihi, Shima (2012) anadai kuwa matumizi ya rangi ni kitu muhimu sana katika utunzi wa hadithi za watoto. Anaendelea kudai kuwa ili kielelezo kinachotumika katika kazi ya watoto kieleweke vizuri ni muhimu sana kwa mtunzi kutumia rangi nyingi kwa kadiri inavyowezeka. Katika uchoraji wa wahusika wa kazi mbalimbali za Vibonzo Jongevu, suala la matumizi ya rangi nyingi za kuvutia limepewa umuhimu mkubwa. Lengo na madhumuni ni kuleta hali ya utoto katika kazi hizi na kuivuta hadhira. Kupitia kazi teule imebainika kuwa suala la rangi limejitokeza katika njia kuu nne. Mosi, ni kupitia mavazi ya wahusika ambao mara nyingi huvishwa nguo zenye rangi mbalimbali na za kuvutia. Ni kawaida kabisa kuona mhusika mmoja akivalishwa nguo zenye rangi zaidi ya moja. Pili, kupitia uumbaji wa mandhari inayowazunguka wahusika.

Tatu, rangi hutumika kuonesha dhana ya jinsia kwa kuonesha rangi zinazopendwa na watoto/watu wa kiume na wa kike. Kwa mfano, uvaaji wa Dora (begi na fulana ya rangi ya pinki) unanasibishwa na uvaaji wa kike. Na nne, rangi hutumika kama sehemu ya maudhui muhimu kwa watoto. Yaani watunzi hulenga

kuwafunza watoto tofauti mbalimbali za rangi kupitia maleba ya wahusika na mandhari inayowazunguka watoto.

### Maumbile ya Kitoto ya Wahusika

Semzaba (ameshatajwa) anadai kuwa muonekano wa wahusika ni sehemu muhimu katika kazi ya msanii. Muonekano wa wahusika huweza kudokeza kwa haraka kuhusu fikra, hisia na msimamo wa msanii. Senkoro (ameshatajwa 2011) anaona kuwa wahusika ndiyo roho ya kazi ya msanii, hivyo muonekano wake ni jambo muhimu kwa hadhira. Watunzi wa Vibonzo Jongevu wametilia umuhimu mkubwa suala la muonekano wa wahusika wao. Aidha, utafiti umebaini kuwa suala la muonekano wa kitoto limejidhihirisha katika namna kuu mbili. Mosi, kupitia maumbile yao ambayo watunzi wameyatumia kwa wahusika wenye maumbo madogo yenye sura za kitoto kama vile Akili, Koba, Baraka na Dora.

Hali hii ya kutumia wahusika wenye maumbile ya watoto ni njia muafaka inayowavuta watoto kuitazama kazi husika. Pili, uhusika wa kitoto umejidhihirisha kupitia maleba/mavazi ya wahusika. Watunzi wamewaumba wahusika wao kwa mavazi/maleba ya kitoto. Kwa mfano, mara zote unapomuona mhusika Akili[2] huwa amevalia gauni lenye taswira ya utoto. Pia, anaoneshwa akiwa amesuka nywele kwa mtindo wa Kilimanjaro au Ukili wa Roza. Mahenge (ameshatajwa) anaiona mbinu hii kuwa ni maalum na inalenga kuleta utambulisho kwa mtazamaji. Ni wazi kuwa utambulisho unaosemwa hapa ni ule wa kumtambua mhusika kama mhusika mtoto. Kwa jicho la kinadharia uchoraji huu wa wahusika unalenga kutengeneza muonekano chanya wa wahusika mbele ya watazamaji (watoto). Hii ni kwa kuwa uumbaji wa wahusika kwa kuwafanya wafanane sana na mtoto wa kawaida, hulenga kuiaminisha hadhira kuwa nao ni sehemu ya kazi husika. Ndio maana hata katika *Dora the Explorer* mhusika Dora[3] daima amechorwa akiwa amevaa kikaptula na begi lake mgongoni. Pamoja na kuwakilisha dhana ya motifu ya kimsako, kwa sehemu kubwa muonekano wa Dora unaakisi dhana ya utoto kupitia umbile lake na mavazi.

### Matendo ya Wahusika

Mara nyingi wahusika wa Vibonzo Jongevu hupewa matendo maalum ambayo kwa kiasi fulani hudhihirisha utoto wao. Kwa mfano, wahusika wengi wa Vibonzo Jongevu wamepewa utendaji mwingi sana wa *kihekaheka*. Hali hii ya

[2] Akili ni mhusika mkuu wa *Akili and Me.* Kazi hii imetengenezwa nchiniTanzania na kwa sasa inaonekana dunia kote kupitia mtandao wa Youtube.

[3] Dora ni mhusika mkuu wa *Dora the Explorer*. Kazi hii imetengenezwa nchini Marekani. Inaonekana kupitia kisimbuzi cha DSTV na kupitia mtandao wa Youtube.

kufanya mambo mengi na kutotulizana katika sehemu moja hudhihirisha tabia halisi ya watoto, hivyo, inapojitokeza katika kazi inawafurahisha sana watoto. Ojiambo (2004) na Bakize (ameshatajwa) wanaona kuwa michezo mingi na kutotulizana sehemu moja ni tabia halisi za watoto na humpasa mtunzi wa kazi za watoto kuzingatia hali hii katika utunzi wake. Kwa mfano, mhusika kama Dora katika kazi zote za *Dora the Explorer* toka anapoianza safari mpaka anapoimaliza daima hatulii. Anapita katika vikwazo mbalimbali na kushiriki katika matukio yote muhimu kuanzia mwanzo hadi mwisho wa simulizi.

Aidha, dhana ya uhusika wa kitoto hujitokeza kupitia hali ya kufanya mambo mbalimbali ya kimajaribio na kwa kukoseakosea. Wataalamu wa makuzi ya watoto wanaamini kuwa ni hali ya kawaida kwa watoto kufanya majaribio ya vitu mbalimbali kwa kuwa hawaogopi kukosea. Majaribio haya huyafanya kwa lengo la kufahamu undani wa jambo/kitu husika. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, katika umri huo watoto wapo katika mchakato wa kujifunza kwa lengo la kuyamudu mazingira yanayowazunguka. Kwa kiasi kikubwa watunzi wa Vibonzo Jongevu wameweza kuakisi hali hii. Kwa mfano, katika simulizi ya 'Desimali Kisimani: Kujumlisha na Kutoa Desimali' ya *Ubongo Kids* tunamuona Akili na rafiki zake wakijaribu idadi tofauti ya watu katika usafiri wa parachuti. Katika majaribio yao wanagundua kuwa upo uzito maalum ambao unaruhusiwa katika usafiri huo na kama ukizidishwa basi hawataweza kuutumia usafiri wao.

Vilevile, kazi kama vile "*The Café"* ya *The Adventures of Abney and Teal* wahusika wake wamechorwa katika hali ya kujaribu kila kitu. Wahusika wakuu ambao ni Abney na Teal wanaonekana wakijaribu kushindana na upepo au kukaa katika mapovu ya maji. Ijapokuwa majaribio yao haya mawili ya kuchekesha yanashindwa lakini ni wazi kuwa wanafanikiwa kuonesha utoto kupitia hali ya ujaribizi. Pia, dhana ya utoto katika matendo ya wahusika inajionesha kwa namna wahusika wanavyokosea mara kwa mara. Kwa mfano, katika *The Cafe* Mara nyingi tunamuona Abney akijikwaa na kuanguka. Wahusika wa katika onesho hili wanaanguka na kumwaga vyakula mara kwa mara hali inayoibua ucheshi kwa watazamaji na kuibua hali ya utoto. Chikaka (2017) anaona kuwa kwa watoto, kitendo cha kuanguka ni jambo la kawaida kutokana na hali yao ya ima kutokuwa makini wakati wa kutembea au hali ya kujifunza namna ya kutembea. Kwa namna zote mbili, hali ya kuanguka mara kwa mara huakisi hali ya utoto. Watoto wanapowatazama wahusika wa Vibonzo Jongevu wakianguka mara kwa mara wanafurahi na wanauona utoto kupitia tendo hili. Pamoja na michezo mbalimbali, dhana hii hujitokeza kwa kupitia matendo kama vile kuimba, kupiga ngoma na ala nyingine za muziki. Pia, ni kawaida kuwaona wahusika hawa wakikimbia, kurukaruka na kufanya kazi nyingine za mikono kama vile kulima na kufua.

**Dhamira za Kitoto**

Dhamira maalum za kitoto vilevile ni njia inayotumiwa na watunzi wa Vibonzo Jongevu katika kuivuta hadhira. Kama ilivyoelezwa hapo nyuma, kazi yoyote ile ya kisanaa huwa na lengo la kuelimisha na kuburudisha hadhira. Imebaini kuwa, watunzi wa vibonzo teule wameweka msisitizo maalum katika dhamira zinazowahusu watoto. Wasanii hawa wamekuwa wakiwabebesha wahusika wao dhamira maalum zinazoakisi dhana ya utoto na watoto wenyewe. Baadhi ya mambo ambayo hujadiliwa sana katika kazi hizi na ambayo ni muhimu kwa watoto ni pamoja na umuhimu wa lishe bora (unywaji wa maziwa na maji safi na salama, na ulaji wa vyakula vingine muhimu vya kujenga mwili kama mayai, samaki na mboga za majani), utunzaji wa mazingira, usomaji wa vitabu vya hadithi za watoto, heshima kwa wazazi, umuhimu wa kupenda shule na safari za kitalii.

Dhamira nyingine zinazojitokeza sana katika kazi za Vibonzo Jongevu ambazo huakisi dhana ya utoto ni pamoja na masuala ya usafi kama vile kupiga mswaki, umuhimu wa kunawa mikono kabla na baada ya kula na baada ya kutoka chooni, utii na heshima kwa wakubwa, kuwapenda wanyama na viumbe wengine, ushirikiano na watoto wengine. Kinadharia ni jambo lililo wazi kuwa Fasihi ya Kidijiti imepata mwitiko mkubwa katika jamii kwa kuwa inalenga kumpa mtoto elimu kwa njia ya burudani. Wazazi, walimu pamoja na watoto wanamtazamo chanya kuhusu Vibonzo Jongevu kwa kuwa vina mambo mengi mazuri yanayohitajika katika makuzi ya mtoto. Aidha vinaweka, msisitizo katika kujifunza kuhesabu, herufi, tofauti za maumbo, sayari na mabadiliko ya usiku na mchana. Imebainika kuwa, wapo watunzi wa Vibonzo Jongevu ambao wamekuwa wakiwaumba wahusika maalum na kuwapa dhamira maalum. Kwa mfano, mhusika Diego katika *Dora the Explorer* yeye amepewa kazi maalum ya kuokoa wanyama walio katika hatari ya kuumia. Mama Ndege katika Ubongo Kids amechorwa kama mtu mwenye kupenda kutoa ushauri na mpishi katika sherehe mbalimbali.

Aidha, uhusika wa kitoto unajitokeza kupitia dhamira za kinjozi. Wataalamu kama Madumulla, Ojiambo, Bakize Shima, Mwashota na Chaula (wameshatajwa) wanaona kuwa, hadhira ya watoto hupenda sana wahusika wao wanapowakilisha na kubeba dhamira za kinjozi/fantasia[4]. Watunzi wa Vibonzo Jongevu wametoa msisitizo mkubwa katika kuonesha dhamira za kinjozi kama njia ya kuivuta hadhira. Kwa mfano, kazi zote za *Adventures of Abney and Teal*

---

[4] Dhamira za kinjozi/fantasia hujumuisha matendo au mambo ambayo hayawezi kutokea katika ulimwengu wa kawaida. Miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na kupaa, kufufuka n.k.

zinaonesha mambo ambayo hayayumkiniki katika akili za kawida. Wanapoanza hadithi zao wanaonekana Abney, Teal na Neep wakishuka kutoka angani kwa usafiri wa mapovu (*bubbles*). Katika hali ya kawaida, kitu hiki hakiwezi kutokea labda katika ulimwengu wa ndoto. Vilevile, wahusika hao wanapotaka kusafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine hutumia povu kama chombo cha usafiri hali inayochekesha na kuongeza mvuto kwa hadhira ya watoto. Aidha, hali hii ya kinjozi inajitokeza katika kazi mbalimbali za Ubongo Kids. Kwa mfano, Akili anasafiri kwenda na kurudi Lala Land kwa kutumia upinde wa mvua. Ingawaje hatumuoni namna anavyosafiri, lakini mara zote anapoingia katika upinde anapotea kimaajabu na ghala anapoibuka huwa ameshafika katika safari yake. Hivyo basi, ni wazi kuwa kuna unjozi mwingi katika matendo ya wahusika tuliowadondoa –katika safari zote mbili zilinukuliwa katika aya hii kwa kuwa safari za Akili na Abney na Teal sio safari za kawaida.

### Uchanganyaji wa Wahusika

Moja ya sifa muhimu inayowavuta sana watoto ni hali ya kuwachanganya wahusika wa kazi zao wanazozitazama. Mara nyingi kazi za watoto hutumia wahusika wanadamu, wadudu, ndege na wanyama. Lyimo (ameshatajwa) anaona kuwa, mbinu hii ya kuchanganya wahusika ni kongwe na hutumika katika tanzu zote za fasihi. Vibonzo Jongevu vinawalenga watoto na uchanganyaji wake wa wahusika una namna yake maalum ambayo hutofautiana sana na kazi za watu wazima. Kwanza, wahusika wasio na sura za kibinadamu mara nyingi ni wengi kuliko wale wenye sura za kibinadamu. Kwa mfano, katika kazi za *Dora the Explorer*, wahusika wa kibinadamu wanaojitokeza mara kwa mara ni Dora na Diego pekee. Wahusika wengine waliobakia wana sura za wanyama mfano Boots (tumbili), Benyy (ng’ombe), Tico (nguchiro), Swipper (Mbweha) n.k.

Pili, katika Vibonzo Jongevu wahusika wasio wanadamu maumbile na muonekano wao hubadilishwa sana na kukaribiana na maumbile ya kibinadamu. Kwa mfano, katika Adventures of *Abney and Teal* mhusika Neep pamoja na kuwa ni mmea (anafana sana na kitunguu) ameumbwa kwa kuwekewa macho, midomo, pua, masikio, mikono na miguu ili umbo lake lifanane na mwanadamu. Sehemu nyingine ya mwili wake imeachwa bila kufinyangwa ili kutopoteza utambulisho wake wa asili la kitunguu. Pia, mhusika Swipper (Mbweha) na Boots (Tumbili) katika *Dora the Explorer* mara zote wanaonekana wakitembea kwa kutumia miguu miwili badala ya kutumia miguu minne kama wanyama wengine. Aidha, miguu yao ya mbele hutumika kama mikono. Hali hii hufanywa kwa lengo maalum la kuleta ukaribu wa wahusika hawa na watu wa kawaida bila kupoteza utambulisho wao wa awali yaani kuwa ni wanyama.

Tatu, wahusika wengi ambao si wanadamu wamepewa uwezo mkubwa wa kuongea na kutenda kuliko hata watu wa kawaida. Kwa mfano, mhusika kama Mama Ndege na Boots wamepewa sifa ya kuwa na maneno ya hekima na busara

kuliko watu wa kawaida. Aidha, mhusika Boots amepewa uwezo wa kuzungumza lugha mbalimbali kama vile Kiingereza, Kihispania na Kichina. Ojiambo na Abdallahh (wameshatajwa) wanaona kuwa mapenzi ya watoto kwa wahusika wanyama ni jambo la asili. Wanaendelea kudai kuwa watoto hupenda kucheza nao na kuongea nao, hii ni kwa kuwa katika umri wa mwanzo wa utoto, watoto huongea na kila kitu wakiwemo wanyama. Hivyo, hali ya kuwajumuisha wahusika katika kazi zao huakisi dunia ya watoto kwa kiasi kikubwa.

### Kusawiri Wahusika Wagunduzi

Vibonzo Jongevu kwa makusudi kabisa husawiri matukio na wahusika wagunduzi kwa lengo la kuivuta hadhira ya watoto. Watunzi wengi wanafahamu kuwa hadhira ya watoto kwa asili wanapenda kazi zenye kutumia motifu za kimsako zenye madhumuni ya kubaini mambo mbalimbali. Bakize, Lyimo na Madumulla (wameshatajwa) wanaona kuwa, masimulizi ya kimsko ni miongoni mwa sifa muhimu ya kijadi inayotumika katika kazi za watoto. Aidha, wataalamu hao wanadai kuwa, mbinu hii hutumika kwa lengo la kujenga taharuki na kuibua mambo mapya miongoni mwa hadhira ya watoto**.** Kwa muktadha huohuo, watunzi wengi wa Vibonzo Jongevu wameitumia mbinu hii katika kazi zao kwa lengo la kuiteka hadhira ya watoto na kuibua mambo mbalimbali ambayo watoto hawayajui. Kwa mfano, katika kazi zote za *Dora the Explorer* simulizi lake kuanzia mwanzo hadi mwisho limejengwa katika safari ya kimsako. Mara zote simulizi linapoanza mtazamaji huambiwa jambo fulani kuhusu safari mhusika mkuu (Dora) na changamoto mbalimbali anazotarajiwa kukutana nazo vilevile hubainishwa.

Hali hii hujenga taharuki na hamu kwa mtazamaji na kuifanya hadhira kuwa makini na kungoja kwa kwa hamu matokeo ya safari husika. Pia, uchoraji wa motifu ya kimsako umejitokeza katika kazi za *Ubongo Kids* kupitia safari za Akili kuelekea *Lala Land.* Mara zote watunzi wamemchora Akili katika hali ya msako wa jambo fulani muhimu ambalo kwa hakika hulengwa kuwa funzo kuu kwa kazi husika. Kupitia msako huo, maudhui na fani mbalimbali hujidhihirisha kupitia matukio na vitushi mbalimbali. Mara zote Akili akiwa safarini hukutana na marafiki zake kama vile Little Lion, Happy Hipo na Bush Baby. Kupitia wahusika hawa, hadhira hujifunza mambo mbalimbali muhimu. Pamoja na kuwa Akili hapitii katika vikwazo vikubwa kama Dora, lakini safari zake zote huwa na lengo maalum la kujifunza/kusaka jambo fulani jipya. Anapomaliza kujifunza huwa ndiyo mwisho wa hadithi husika.

### Lugha na Sauti za Kitoto

Imebainika kuwa wahusika wengi wa kazi za Vibonzo Jongevu hutumia misamiati, sentensi na sauti maalum za kitoto kama njia ya kuivuta hadhira ya watoto. Pia, hali hiyo hujitokeza kupitia uteuzi wa maneno na namna ya

kuyatamka maneno hayo. Lyimo (ameshatajwa) anaongeza kuwa, ni muhimu pia kwa mtunzi wa kazi za watoto kutumia sentensi fupifupi na maneno yenye staha ambayo yanakubalika katika jamii. Kwa mfano, katika kazi za *Ubongo Kids* mara zinapoanza anasikika msimulizi akisema "Huyu ni Akili. Karibuni ataanza safari yake. Huko atakutana na rafiki zake". Sentensi zilizotumika katika simulizi hili ni fupifupi.

Ngugi (2014) anaona kuwa matumizi ya sentensi fupifupi katika kazi za watoto ni muhimu kwa kuwa huwasaidia watoto kuelewa kwa urahisi simulizi husika. Haitarajiwi katika kazi za Vibonzo Jongevu kuwa na msamiati mgumu na kama itabidi kutumia msamiati fulani maalum basi mtunzi hulitolea maana na kuliweka katika muktadha ambao watoto wanaweza kuelewa kwa urahisi. Aidha, kuna msisitizo maalum wa matumizi ya sauti za kitoto. Kwa kuzingatia kuwa kazi za Vibonzo Jongevu zina sifa ya kusikika na kuonekana (*audio visual*) watunzi wake wameamua kwa makusudi kutumia sauti za kitoto ili kudhihirisha hali ya utoto katika kazi hizo. Pia, ili kulinda utambulisho wa wahusika na kuongea wapenzi wa wahusika hao sauti zao zimekuwa zikilindwa bila kubadilishwabadilishwa[5]. Kuna namna Hali hii huwafanya watoto kuwajua na kuwazoea wahusika hawa hali inayojenga mapenzi makubwa baina ya watoto na kazi za Vibonzo Jongevu.

### Uhusika Hai

Uhusika hai katika muktadha wa makala haya umetumika kuelezea hali ambapo wahusika huishirikisha hadhira katika kazi ya sanaa. Sio jambo la kawaida, lakini hali hii hujitokeza mara kwa katika utunzi wa kazi za Vibonjo Jongevu kwa wahusika wake kuuliza maswali kwa hadhira na kuhitaji majibu. Pia, wakati fulani fulani wahusika hawa hasa wapokuwa na shida au hali ya utata wa kuamua kuchagua jambo moja katika ya mambo mengi huomba msaada kwa hadhira ili iwasaidie kufanya uchaguzi mzuri. Aina hii mbili ya ushirikishwaji wa hadhira ni athari ya wazi kutoka katika fasihi simulizi - ambayo inafahamika wazi kuwa hadhira yake ni hai kwa kuwa inatumia wahusika hai ambao wanaathiriwa na ushiriki wao katika simulizi. Kwa kuzingatia namna ya kipekee mhusika Dora ametia fora kwa kuishirikisha sana hadhira yake. Mara zote Dora huwa na chaguo zaidi ya moja na huiomba hadhira yake imsaidie kuchagua. Pia, huuliza maswali kadha wa kadhaa kwa hadhira na husubiri muda kidogo ili kuwapa fursa watoto kutoa majibu yao kisha yeye (Dora) hutoa Jibu Lake. Hali hii sio tu hutoa fursa

[5] Sauti pamoja na muonekanao wa wahusika wa Vibonzo Jongevu ni utambulisho (*brandy*) za kibiashara na zimekuwa zimekuwa zikiwafaidisha sana watunzi (Rejea ABdallah 2018).

kwa watoto kushiriki kwa kujibu au kufanya uchaguzi wa mambo lakini pia huongeza usikivu wao katika kazi wanazozitazama.

### Umuhimu wa Uhusika wa Kitoto kwa Hadhira ya Watoto

Ni dhahiri kuwa, mbinu tajwa zimeongeza hali ya watoto kuzipenda na kujiona ni sehemu ya umiliki wa kazi za Vibonzo Jongevu. Ojiambo (ameshatajwa) anaamini kuwa, ni muhimu kwa mtunzi wa kazi za watoto kuijenga kazi yake katika hali ambayo hadhira yake itajiona kuwa ni sehemu muhimu ya kazi husika. Aidha, Lyimo (ameshatajwa) anaona kuwa ili mwandishi aweze kuufikisha ujumbe wake vizuri kwa jamii anapaswa kuijua hadhira yake na kuandika kwa lugha ambayo wanaweza kuisoma na kuelewa. Ndio maana watunzi wa Vibonzo Jongevu wametumia mbinu mbalimbali ili kutengeneza hali ya utoto na kuifanya hadhira ijione kuwa ni sehemu ya kazi husika. Kwa mfano, watunzi wa Ubongo Kids na *Dora the Explorer* wanalazimika kutumia sauti za kitoto, michezo ya kitoto na kujadili dhamira za kitoto. Katika hali hiyo basi, watoto huvutiwa na kinachowasilishwa.

Utafiti umebaini kuwa matumzi ya wahusika wa kitoto husaidia ujumbe wa msanii kufika vyema kwa hadhira yake. Shima, Madumulla na Bakize (wameshatajwa) wanaamini kuwa, uchoraji mzuri wa wahusika husaidia ujumbe wa msanii kueleweka kwa urahisi. Aidha, Ngugi (ameshatajwa) anaona kuwa uhusika wa kitoto hulenga kuleta mvuto maalum kwa hadhira inayotazama. Aidha, utafiti umebaini kuwa hali ya utoto inayoonekana katika kazi mbalimbali za Vibonzo Jongevu imeongeza mapenzi makubwa kwa kazi za Vibonzo Jongevu. Kinadharia, hali hii ni ishara nzuri kwa ukubalifu wa sanaa hii mpya kwa hadhira ya watoto na jamii kwa jumla. Ni wazi kuwa watoto wanaonekana kuzipenda kazi hizi kwa kuwa zinakidhi haja ya kuwaelimisha na kuwaburudisha. Ndiyo maana kwa namna ya kipekee watunzi wa Vibonzo Jongevu wanalitazama kundi la watoto kama kundi maalum lenye fikra, msimamo na falsafa inayowatambulisha kama kundi maalum la kijamii. Hivyo, wanatumia fursa hii kuwaunda wahusika wa kitoto kwa minajili ya kufikisha ujumbe wao kwa hadhira hii.

### Hitimisho

Wahusika wa Vibonzo Jongevu kama walivyo wahusika wa kazi nyingine za fasihi ni sehemu muhumu katika kazi za Vibonzo Jongevu. Wahusika hubeba fikra, hisia, falsafa, msimamo na maoni ya msanii. Wahusika huibeba fani na maudhui ya mtunzi. Mara nyingi watunzi wa kazi za Sanaa huwalenga watoto kama kundi maalum, hivyo huwatumia kwa namna ya kipekee wahusika hawa katika kuufikisha ujumbe wao kwa hadhira. Vilevile, watunzi hujaribu kuwajenga wahusika wao katika hali ya utoto ili kuleta hali ya utoto katika kazi zao. Kwa

kufanya hivyo, kazi hizi zimekuwa na mvuto mkubwa na zinazidi kuwa maarufu miongoni mwa hadhira ya watoto.

**Marejeleo**

Abdallah, S. (2018). "Nafasi ya Fasihi ya Kidijiti katika Kukuza Fasihi Simulizi: Mifano Kutoka katika Vibonzo Jongevu". Tasinifu ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Maccony Printing Press.

Chikaka, J. K. (2017). *Watoto na Ndoto za Maisha*. Dar es Salaam: DeskTop Production.

Jylha-Laide, J. (2006). Leaning by Viewing: Cartoon as Foreign Language Learning Materials for Children - A Case Study, *Journal of Education Television*, 20 (2).

Kasiga, G. (2013). "U-Nigeria Katika Filamu za Tanzania: Chanzo Chake, Sababu za Kutumiwa na Athari zake kwa Wa-Tanzania." Tasnifu ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Lyimo, E. B. (2014). Nduni za Fasihi ya Watoto: Mifano Kutoka katika Vitabu vya Kiswahili ya Fasihi ya Watoto Nchini Tanzania" katika *Mulika* Juzuu ya 33. Uk. 33-45.

Madumulla, J.S. (2001), Hali ya Vitabu vya Watoto katika Tanzania, katika *Swahi1i Forum* Juzuu ya 8. Uk. 171-183.

Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.

Mahenge, E. (2017). *Filamu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Lulu.

Mazzavella, S. R. (2007), *20 Questions About Youth and Media*. New York: Peter Lang.

Mlaga, W. K. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Mrikaria, S. E. (2007). Fasihi Simulizi na Teknolojia, katika *Swahi1i Forum* Juzuu ya 14. Uk. 197-206.

Mulokozi, M. M. (1989). Tanzu za Fasihi Simulizi, katika *Mulika*, Juzuu 21. Uk. 1-24.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Ngugi, P. M. (2011). Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya, katika *Kioo cha Lugha,* Juz. 9, Kur. 84-94.

Ojiambo, B. T. (2004). "Uhakiki wa Tamthiliya ya Watoto kama zao la Michezo ya Utotoni". Tasnifu ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa).

Ponera, A. S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Printing Technlogy.

Semzaba, E. (2006). *Tamthilia ya Kiswahili*, (Tol 2). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTU.

Shima, G. (2012). "Nafasi ya Vielelezo katika Fasihi ya Watoto". Tasnifu ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).